MEDICAL STRIP CARTOON collection

# JUMA NA KiCHOCHO



This document was produced with technical guidance from the Training Unit (TDT) and the Schistosomiasis and Intestinal Parasites Unit (SIP) of the Division of Control of Tropical Diseases (CTD), World Health Organization and based on an original design by CHADU.

Mfasiri : Dkt. Jean de Dieu KARANGWA, mwalimu katika INALCO (Institut National des Langues et Civilisations Orientales), Paris.

WORLD HEALTH ORGANIZATION
Division of Control of Tropical Diseases
WHO / CTD

CHADU

Creation and edition of health educative material

unicef

Reproduced with UNICEF financial support

MEDICAL STRIP CARTOON collection

# JUMA NA KICHOCHO




JUMA WATOTO WENGINE WA KIJIJI WANAKWENDA SHULENI....
SHULE
KICHOCHO
LEO TUTAZUNGUMZIA KICHOCHO, NANI ANAJUA KICHOCHO NI NINI? NDIYO, WEWE JUMA!
NI UGONJWA UNAOSABABISHWA NA MINYOO WADOGO WANAOINGIA KATIKA NGOZI.
UNAJUA MAHALI AMBAPO WANAPATIKANA?
WANAPATIKANA KATIKA MITO NA MADIMBWI, LAKINI NI WADOGO SANA NA HUWEZI KUWAONA.


MINYOO HAWA WANAWEZA KUTUAMBUKIZA UGONJWA, NI MAADUI WETU NA INABIDI TUJIUNGE PAMOJA ILI TUPAMBANE NAO.
WANAINGIA VIPI MITONI?
NA TUNAWEZAJE KUWAZUIA KUINGIA MIILINI MWETU?
WATU AMBAO NI WAGONJWA HUPITISHA MAYAI YA MINYOO KATIKA MKOJO NA HAJA KUBWA MAJINI WANAPOKOJOA AU KWENDA HAJA KUBWA NDANI AU KARIBU YA MITO NA MADIMBWI.
MAYAI YANAANGULIWA KATIKA MAJI NA MINYOO WADOGO SANA WANAONDOKA KUTOKA NDANI YAKE NA KUWA KONOKONO, MINYOO HAWA WANAKUA KATIKA KONOKONO.


MNYOO ANAPOONDOKA KUTOKA KWENYE KONOKONO, BADO NI MDOGO SANA...
HUWEZI KUMUONA...
LAKINI, ANAWEZA KUPITA KATIKA NGOZI YA WATOTO WANAOCHEZA NA KUOGELEA KATIKA MITO NA MADIMBWI... AU... WAKATI WATU WAZIMA WANAPOFANYA KAZI KARIBU AU NDANI YA MAJI.
WANAISHI WAPI KATIKA MWILI WETU?.. JE, WANAISHI KATIKA NGOZI?
HAPANA!.. MWILINI, MINYOO HAWA WANAKUA NA KUWA WAREFU KAMA UKUCHA WA KIDOLE... WENGINE HUISHI KATIKA UTUMBO NA WANAWEZA KUSABABISHA KUUMWA TUMBO NA KUHARISHA (MARA KWA MARA NDANI YA CHOO MNA DAMU). MTU MGONJWA HUSIKIA UCHOVU NA HAWEZI KUCHEZA AU KUFANYA KAZI VIZURI...


WENGINE HUISHI KANDOKANDO YA KIBOFU. WATU AMBAO WANA AINA HIYO YA MINYOO WANAHITAJI KUKOJOA MARA NYINGI NA MARA KWA MARA WANAUMWA WANAPOKOJOA. MARA KWA MARA PIA MKOJO WENYEWE NI WA RANGI NYEKUNDU (MNA DAMU NDANI)... MTU HUJISIKIA PIA MGONJWA...
MWANZONI MWA UGONJWA MTU YU MZIMA.
... KWA HIYO SI WABAYA SANA KWETU!
JIHADHARI !!.. NI HATARI KWA SABABU WANAISHI KATIKA MILI YETU BILA SISI KUWASIKIA... LAKINI WANASABABISHA BAADAYE UGONJWA WA HATARI !!! NA WANASHAMBULIA WOTE, VIJANA, WAZEE, WAVULANA WASICHANA...


NA TUNAWEZA KUFANYA NINI ILI TUWAZUIE MINYOO KUINGIA MTONI ?
¡NGEFAA TUSIENDE HAJA NDOGO WALA KUBWA KARIBU AU NDANI YA MTO !
HILI NI JAMBO MUHIMU NA HAMNA BUDI KUWAAMBIA PIA WENGINE... JE VIPI TUNAWEZA KUZUIA MINYOO KUINGIA KATIKA NGOZI ZETU ?
JARIBUNI KUTOCHEZA AU KUTOOGA NDANI YA MITO NA MADIMBWI


LAKINI NIKIVAA NGUO ZANGU, NINAWEZA KUTOPATA UGONJWA HUO !
LA HASHA !!! MAJI MACHACHE MWILINI YANATOSHA ILI UAMBUKIZWE
TUTAONANA NYOTE KESHO... KUMBUKENI MANENO NILIYOYASEMA ... OGENI MAJI KUTOKA VISIMANI AU MABOMBANI... NA CHEZENI UWANJANI.
NITACHEZEA MTONI. SIOGOPI MNYOO MDOGO!
LA, LUKA ACHA TUCHEZEE KARIBU NA NYUMBANI KWETU.
TAZAMA! JUMA! BABA ANAFANYA NINI?
HIYO NI NINI BABA?
TUNAJENGA CHOO CHA FAMILIA YETU.


AHA, NI VIZURI! TUNAWEZA KWENDA HAJA HAPA NA HATUTARUDI KARIBU NA MTO!
ULISIKIA MARIAM? HATUNA BUDI PIA KUCHEZA KARIBU NA NYUMBA AU UWANJANI, TUSICHEZEE TENA MTONI.
JUMA!
JUMA, TAFADHALI MPELEKEE CHAKULA HIKI BABU YAKO SHAMBANI... UWE MWANGALIFU KARIBU NA MTO.
ALIPOKUWA AKITEMBEA KANDO YA MTO, JUMA AKAKUTANA NA RAFIKI YAKE LUKA
UNAFANYA NINI LUKA ?
OOO, NINAKWENDA KUCHEZA NDANI YA MTO!


HAPANA, USIFANYE HIVYO!!
KUMBUKA MWALIMU ALIVYOSEMA!! USICHEZEE MTONI. KWA SABABU NI VIBAYA PIA KWETU NA KWA WANAKIJIJI WOTE KAMA TUNAENDELEA KWENDA HAJA NDOGO NA KUBWA KANDO YA MTO.
KAKA YAKO YUKO PAMOJA NAWE. UNATAKA APATE KICHOCHO?


MWALIMU ALISEMA KUWA MTO WETU UMEJAA MINYOO WADOGO SANA WANAOSABABISHA KICHOCHO...
...MINYOO WADOGO WANAKUA KATIKA KONOKONO HAWA NA HUACHWA HURU KILA SIKU NDANI YA MAJI.
NILIMSIKIA MWALIMU AKIMWAMBIA BABA KUWA TUKIWEZA KUUA KONOKONO WOTE MITONI NA NDANI YA MADIMBWI, HIVYO TUNAWEZA KUZUIA KICHOCHO ... LAKINI ALISEMA KUWA NI VIGUMU SANA... KWA HIVYO NI BORA KWETU KUBADILI BAADHI YA TABIA ZETU...



LUKA, TAZAMA!!! MUSA ANA MKOJO MWEKUNDU!! LABDA ANA KICHOCHO?
UNA HAKIKA?
PAPO HAPO, MWALIMU ANAPITA KARIBU AKITOKA SHAMBANI NA ANASIKIA MANENO YANAYOHUSU MKOJO MWEKUNDU.
NINAJUA KUWA HIVI KARIBUNI MTU KUTOKA KITUO CHA AFYA ATAKUJA KUTUTEMBELEA, WAKATI HUO TUTAJUA KUWA MUSA ANA KICHOCHO.
KAMA ALIVYOSEMA MWALIMU, SIKU CHACHE BAADAYE, WATU KUTOKA KITUO CHA AFYA WALIKUJA NA KUPIMA WATOTO WOTE. WATOTO HAWAKUWA NA BUDI KULETA CHOO KIDOGO NA CHOO KIKUBWA ILI VIPIMWE.
LUKA!! TAZAMA HAPA, WEWE NA MUSA MNA KICHOCHO!


WEWE NA MUSA CHUKUENI DAWA HII HAPA. ITAUA MINYOO MWILINI MWENU NA MTAPATA NAFUU HARAKA. LAKINI KUMBUKENI! MSICHEZE NDANI YA MTO, NI RAHISI KUPATA KICHOCHO TENA NA KUWA WAGONJWA!
KWA HIYO... MKITUMIA VYOO NA KUACHA KUCHEZEA NDANI YA MITO NA MADIMBWI, TUTAWEZA KUONDOA KICHOCHO HARAKA KIJIJINI MWETU. PIA WAAMBIENI MAMBO HAYA WAZAZI WENU, BABU BIBI NA NDUGU ZENU WENGINE ... HATUNA BUDI SOTE PAMOJA KUPAMBANA NA KICHOCHO. NA NI KWA NJIA HIYO PEKEE TUTAWEZA KUSHINDA.
KICHO
KICHOCHO
LUKA, NJOO, UNAJISIKIA VIZURI ZAIDI? HEBU TUCHEZE KANDANDA!
KICHOCHO KINAWEZA KUZUILIWA IKIWA WATU WOTE KIJIJINI WATASHIRIKI. UJUMBE WA KUTOTUMIA MAJI YALIYOINGIWA MINYOO NA KUACHA KUCHAFUA MTO KWA MKOJO NA HAJA KUBWA UNGEZINGATIWA NA KILA MMOJA. KAMA VILE KATIKA KIJIJI CHA JUMA, HII INGESAIDIA KUONDOA HARAKA KICHOCHO.




© 1997 - CHADU

3, quai Joseph Gillet - 69004 LYON - FRANCE
Tél. (33) 4 72 39 08 21 - Fax (33) 4 72 39 21 05

Concept and design by CHADU
Law n° 49-956 du 16 juillet 1949
First published, 4th Trimester 1997
ISSN : 1159-9294
ISBN : 2.909.412.27.X





